## Jimbo la Nyahururu

Mwaka huu 2020, kuna mambo kadhaa muhimu katika maisha ya Jimbo letu tunayostahili kukumbuka:

- **Mchango wa mwaka 2020** kwa ajili ya Jimbo la Nyahururu umeshagawiwa kati ya Parokia za Jimbo. Ni jukumu la kila Mkristu kuchangia kulingana na uwezo wake kwa ajili ya kusimamia mahitaji ya Kanisa.
- Jumamosi 28 Machi, itakuwa siku ya kutimiza **miaka 17 ya Jimbo la Nyahururu**. Kutakuwa na Ibada ya Shukrani Nyahururu, kule kwa Secretariat.
- Sherehe nyingine itafanywa Jumamosi 9 Mei, kwa **kufungua rasmi nyumba mpya ya Baba Askofu**, kule Nyahururu. Ibada na baraka itaongozwa na Kadinali John Njue, Askofu Mkuu wa Nairobi.
- Siku ya **Harambee kwa ajili ya miradi ya maendeleo ya Jimbo**, mwaka huu itakuwa Jumamosi 29 Agosti.
- Kisha, Wakatoliki wote wa nchi wamealikwa kule Subukia kwa ajili ya **Siku ya Maombi ya Kitaifa** Jumamosi 3 Oktoba, inayopangwa na Maaskofu wa Kenya. Kama kila mwaka, hiyo ni siku muhimu sana ya kukutana pamoja Wakristu wa kila Jimbo pamoja na wachungaji wetu.

*HABARI FUPI*

### Vyama

**CA** - Jumamosi 21 Machi kutakuwa na safari ya kidini ya wanachama wote wa Ng'arua Deanery kwenda Nanyuki. Mkutano wa wachama wote utakuwa Jumatano 1 Aprili.

**CMA & CWA** - Wanachama wanaendelea kujiandikisha kwa mwaka huu, na kujitayarisha kwa siku ya Nadhiri, zitakazofanywa pamoja Jumapili ya Parish Baraka Day, 26 Aprili.

### Scouts

Viongozi wote wa Maskauti wa Parokia walifanya Camp kule Ol Motunyi, Ijumaa 24 hadi Jumapili 26 Januari, wakasoma kuhusu mbinu na kazi zao na kupanga utaratibu wa chama.

Tena, kuanzia Ijumaa 21 hadi Jumapili 23 Februari, waakilishi wa kila sehemu ya kikundi walihudhuria sherehe ya Founder's Day, kule Nyeri, ambapo Maskauti hukusanyika kusherehekea siku ya kuzaliwa ya mwanzilishi wa Scouts, Sir Robert Baden Powell, aliyezikwa Nyeri.



### PMC

Promoters wa PMC wa Ng'arua Deanery walikutana hapa Ol Moran Ijumaa 21 Februari. Fr. John Karatu, aliye mratibu wa PMC katika Jimbo la Nyahururu, aliwasomesha kuhusu huduma yao kwa ajili ya watoto, na kuhusu maisha ya Kikristu.

Watoto wa PMC wameanza kuchangisha Pro-Forma kwa ajili ya kuongeza hazina yao na kuchangia mradi wa PMC ya Jimbo. Kwa sababu hiyo, wanapanga sherehe na harambee ya PMC ya Kiparokia itakayofanywa mwezi wa tano, tarehe 31. Tena, watoto wameanza kujifunza za mashindano ya PMC katika Makanisa.

### Vijana

Vijana wa Parokia wanamalizia kufanya Registration ya Jimbo ya mwaka 2020. Ijumaa 6 Machi Patrons na Matrons wa kila Kanisa Dogo watakutana Ol Moran kwa kupanga kazi ya kikundi na uchaguzi wa viongozi wa Vijana, utakaofanyika mwezi wa tatu.

### Makatekista

Makatekista Wapya (ama Junior Catechists) wanaendelea kufunzwa mambo ya huduma. Hata katika Parish Assembly viongozi wa Makanisa wameombwa watafute Wakristu wanaoweza kufunzwa na kufanywa kuwa Makatekista au Wasaidizi wa Makatekista (Assistant Catechists) katika Makanisa Madogo.

Mwezi uliopita Makatekista wa Parokia walipewa barua rasmi ya uteuzi wa mwaka huu. Waliopewa barua hiyo ni Makatekista wenyewe. Kila Kanisa Dogo litafute pia Wasaidizi wa Makatekista.

Walioteuliwa kama Makatekista ni hawa: *Kabati:* Francis Wambugu; *Mithuri:* John Ndungu; *Minjore:* James Kamugwi; *Githima:* Basilio Ngugi, Peter Mwangi; *Ol Motunyi:* Anastasia Mumbi, Milka Wangu; *Kahuho:* David Ndungu; *Mbombo:* Peterson Muthua, Susan Wamaitha; *Ngare Narok:* Evans Kemo; *Ol Moran:* Francis Njenga, Elizabeth Kore, Veronika Nalubo, Jane Wanjira; *Miharati:* James Thuo, Neemia Wachira; *Magadi:* Evans Muturi, Regina Ekwam; *Survey:* David Munyiri; Posta: Fred Lokale; *Nagum* & *Dam Mbili*: John Wanyama; *Lounyek:* Simon Njoroge; *Ndunyuriwo:* Jacob Ngetich.

#### Utaratibu wa Machi-Aprili 2020

*Jumapili 8 Machi* - ya 2 ya Kwaresima *(Mt 17:1-9)*
→ Misa - 7am: Ol Motunyi; 8am: Minjore; 9am: Kahuho; 10am: Mithuri; 11am: Ol Moran; 12.00: Mbombo
→ 4.00pm: Ol Moran, Masifu ya Jioni

*Jumapili 15 Machi* - ya 3 ya Kwaresima *(Jn 4:5-42)*
→ Misa - 7am: Survey; 9am: Miharati, Ngare Narok; 11am: Ol Moran, Nagum
→ 4.00pm: Ol Moran, Masifu ya Jioni

*Alhamisi 19 Machi* - Sherehe ya Mt. Yosefu, Mume wa Bikira Maria
→ 7.00am: Ol Moran, Misa ya Sherehe

*Jumamosi 21 Machi*
→ 10.00am: Ol Moran, Parish Education Day na Sherehe ya Miaka 10 ya Nyumba ya Wanafunzi 'Hekima House'

*Jumatano 25 Machi* - Sherehe ya Maria Kupashwa Habari ya Kuzaliwa Bwana Yesu Kristu *(Announciation of the Lord)*
→ 7.00am: Ol Moran, Misa ya Sherehe

*Jumapili 22 Machi* - ya 4 ya Kwaresima *(Jn 9:1-41)*
→ Misa - 7am: Kabati; 8am: Gituamba; 9am: Githima; 10am: Posta; 11am: Ol Moran
→ 4.00pm: Ol Moran, Masifu ya Jioni

*Jumamosi 28 Machi*
→ Sherehe ya Miaka 17 ya Jimbo la Nyahururu

*Jumapili 29 Machi* - ya 5 ya Kwaresima *(Jn 11:1-45)*
→ Misa - 9am: Lounyek, Magadi; 10.30am: Dam Mbili; 11am: Ol Moran; 12.00: Ndunyuriwo
→ 4.00pm: Ol Moran, Masifu ya Jioni

*Jumamosi 4 Aprili*
→ 10.00am: Ol Moran, Mkutano wa Makatekista walioteuliwa

*Jumapili 5 Aprili* - Jumapili ya Matawi *(Mt 26:14-27:66)*
*Mwanzo wa Juma Kuu*
→ 10am: Ol Moran, Maandamano ya Matawi na Misa ya Mateso;
→ 10am: Mithuri, Maandamano ya Matawi na Misa ya Mateso;
→ 10am: Magadi, Maandamano ya Matawi na Ibada ya Neno;
→ 10am: Dam Mbili, Maandamano ya Matawi na Ibada ya Neno;
→ 4.00pm: Ol Moran, Masifu ya Jioni

SAUTI *ya Mtakatifu* MARKO
*- No. 79, Year 12, Printed on 5th March 2020 - (NOT FOR SALE)*
**SAINT MARK** CATHOLIC PARISH - Ol Moran - *Catholic Diocese of Nyahururu*
*P.O.Box 20 - 20320 Kinamba* - saintmark@olmoran.it - *+254 720 924 153*
Printed by POP-SIGNS MEDIA
Nairobi - Tel. 0720 845 699 and 0724 236 271

**Mt. Marko Mwinjili na Msimamizi wa Parokia**
*Aliishi Yerusalemu. Baada ya ubatizo wake, akafuatana na Mtume Paulo. Kisha aliishi Roma na Mt. Petro, akaandika Injili akikusanya mafundisho yake. Akaeneza Ukristu na kuanzisha Kanisa Aleksandria ya Misri. Akawa Mhubiri, Askofu na Shahidi wa kwanza kwenye bara la Afrika.*

Gazeti la Parokia Katoliki
ya Mtakatifu Marko Mwinjili ya Ol Moran
*N. 79 — Mwaka wa 12*
**Februari—Machi 2020**

# SAUTI *ya Mtakatifu* MARKO

*Kwaresima 2020: kujitayarisha kiroho kwa Pasaka ya Yesu*

## Uzuri wa Safari ni Mwelekeo

Tumeanza safari ya Kwaresima, yaani kipindi cha siku arobaini za matayarisho ya kiroho kwa sherehe kuu ya Pasaka.

> Hakuna barabara iliyo njema kwa msafiri asiyejua aendapo.

Mfano mzuri wa Kwaresima kweli kweli ni safari. Ndiyo sababu nataka kutumia methali mbili, kwa kufahamu maana ya Kwaresima.

Methali wa kwanza husema: "Uzuri wa safari sio matembezi, bali mwelekeo". Maana, haitoshi kuwa safarini, lazima mtu ajue anapoelekea ili afahamu uzuri wa safari. Safari ni nzuri si kwa sababu tunatembea, bali kwa sababu ya tunapoelekea. Hivyo ni Kwaresima.

Uzuri wa Kwaresima ni mwelekeo wake, yaani Pasaka ya Mateso, Kifo na Ufufuko wa Yesu. Mambo haya ni yale muhimu kuliko yote katika imani ya Kikristu. Sherehe ya Pasaka mwaka huu itakuwa Jumapili 12 Aprili. Tulianza Kwaresima Jumatano 26 Februari. Mwelekeo wa Kwaresima ni Pasaka. Wakati huu tujitolee kwa ukarimu katika matayarisho ya kiroho, kwa njia ya kutubu dhambi na kurekebisha tabia, kwa kujitolea katika huruma, na kusali zaidi. Kwa njia hii tutafika Pasaka na moyo mpya, na Pasaka ya Ufufuko itakuwa baraka na furaha yetu!

Safari ni mfano wa maisha yetu pia. Bila mwelekeo safi, maisha yaanza kukosa ladha yake. Kwa kweli, mtu asiye na mwelekeo hulalamika sana. Kila wakati kuna mambo au watu wanaomsumbua. Hupenda raha, wala hapati furaha ya kudumu.

Hapo nitaje methali ya pili: "Hakuna barabara iliyo nzuri kwa msafiri asiyejua anapokwenda".

Hakuna njia ya maisha inayoleta furaha ya kweli, tusiposhika mwelekeo wa maana. Yesu Kristu alitupatia mfano wa kuufuata katika Pasaka yake, kwa njia ya Msalaba, kwa njia ya huruma. Tufuate njia ya Yesu, tushike mwelekeo wake.

Fr. Giacomo Basso - *Baba Paroko*

*Ibada ya Jumatano ya Majivu Ol Moran, tarehe 26 Februari, mwanzo wa safari ya Kwaresima.*



### KIPINDI CHA KWARESIMA


*Kuanzia tarehe 26 Februari, **Jumatano ya Majivu**, Kanisa limeingia katika Kipindi cha Kwaresima, wakati maalum wa siku arobaini za toba na maandalizi kwa Sherehe Kuu ya Pasaka ya Mateso, Kifo na Ufufuko wa Bwana. Mwanzo wa Juma Kuu itakuwa **Jumapili ya Matawi,** tarehe 5 Aprili, **Jumapili ya Pasaka** ya Ufufuko, tarehe 12 Aprili. Twakumbushwa shughuli za Kwaresima, hasa Parokiani mwetu:*
*- **TOBA:** Kama ishara ya **malipizi**, Jumatano ya Majivu na Ijumaa ya Juma Kuu ni siku za kufunga chakula. Tena, kila Ijumaa ya Kwaresima Wakristu hujinyima nyama. Siku zote za Kwaresima Wakristu huzoea kujinyima anasa na kurekebisha mwenendo. Ni muhimu kupokea **Sakramenti ya Kitubio** kabla ya Pasaka: kutakuwa hata na masomo na nafasi ya Kitubio katika Makanisa Madogo.*
*- **SALA:** Kila Ijumaa, katika kila Kanisa Dogo, Wakristu husali na maombi ya **Njia ya Msalaba**; pia **Masifu ya Jioni**, kila Jumapili, saa kumi, Ol Moran.*
*- **SADAKA: Sadaka Maalum ya Kwaresima**, kwa ajili ya maskini, hutolewa katika kila Ibada ya Kwaresima, kuanzia Jumatano ya Majivu hadi Alhamisi Kuu.*

*Ng'arua Deanery*

### KITABU CHA NJIA YA MSALABA

*Kitabu kipya cha maombi ya Njia ya Msalaba kimetolewa katika Ng'arua Deanery.*

*Kitabu hiki kinatolewa pamoja na vitabu vingine vya maombi mbalimbali, kama kile cha Novena ya Noeli. Vimeandikwa kwa lugha ya Kiswahili, kwa ajili ya Parokia tano za Deanery. Faida ya uuzaji wa vitabu hivi itasaidia hazina ya Deanery.*




***KShs 80/=***

*Viongozi wa Parokia*

## 14th Parish Assembly

*Viongozi wa Parokia nzima walikutana katika Parish Assembly ya 14, Jumamosi 18 Januari. Hiyo ilikuwa mara ya kwanza kukutana kama Viongozi baada ya Uchaguzi wa Kiparokia wa mwaka uliopita.*

*Walijadiliana kuhusu mambo kadhaa yanayohusu maisha ya Parokia:*

*1) Ripoti ya michango ya mwaka 2019,na mpango wa **michango ya mwaka 2020** kwa ajili ya Jimbo la Nyahururu.*

*2) Maendeleo ya Parokia na **Parish Baraka Day**: Mwaka huu mradi wa Parokia utakuwa kurekebisha na kuboresha nyumba za Pastoral Centre, hasa St. Peter's Hall. Gharama ya hizo kazi itachangiwa na sherehe ya Parish Baraka Day, sikukuu ya Msimamizi wa Parokia Mt. Marko Mwinjili, itakayofanywa Jumapili 26 Aprili.*

*2) Uteuzi wa **Makatekista** na wasaidizi wao, pia haja ya kutafuta Makatekista wapya, na kuwafunza.*

*3) **Ziara ya viongozi** wa Halmashauri Kuu kutembelea vijiji vya sehemu za Kaskazini za Parokia yetu.*

*4) Majadiliano kuhusu hali ya **Vijana** na ya **watoto wa PMC** katika Parokia yetu, tena kuhusu haja ya kuongeza Patrons na Matrons wa Vijana, na Promoters wa PMC.*



*Juu:* Viongozi wa Parokia nzima walipokutana katika Parish Assembly ya 14, Ol Moran, tarehe 18 Januari.

*Baada ya Parish Assembly, Viongozi wa Makanisa Madogo walikutana tena Jumamosi 29 Februari, katika Zones nne za Parokia, kwa ajili ya **Semina kuhusu uongozi** wa Kikanisa.*

*Masista Wapya*

## Baraka ya Miito

Hata mwaka huu tumepokea kipaji cha Masista Wapya. Sherehe yao ilikuwa Jumamosi 8 Februari. Baba Askofu Joseph alikuja kuongoza ibada ya Misa Kuu. Mbele yake na mbele ya Sista Mkuu, Sr. Maddalena Ergasti, wasichana watano walifanya Nadhiri za Utawa mara ya kwanza, katika Shirika la Masista "Servants of the Visitation". Hao ni Sr. Angelina Mwende Mang'oka (kutoka Machakos, ametumwa Brasil), Sr. Esther Wanjia Ciira (kutoka Parokiani mwetu, hapo Kahuho, ametumwa Naiorbi), Sr. Jennifer Kanini Musyimi (kutoka Machakos, atahudumu Ol Moran), Sr. Joyce Kathini Dorcas (kutoka Machakos, atahudumu Ol Moran), Sr. Laingo Maminiaina Clemence Raholiarisoa (kutoka Madagascar, ametumwa Brasil). Mapadri wa Parokia, pamoja na Mapadri wengine wageni na Wakristu wengi walijiunga na Masista wetu katika hiyo ibada na katika sherehe iliyofuata. Furaha ya siku ya Nadhiri inaonyesha wazi baraka ya miito katika maisha ya Kanisa.

Tena, jioni ya Ijumaa tarehe 7 Februari, wasichana wengine sita waliingia katika Novitiate, yaani hatua nyingine katika mafudisho ya maisha ya Kitawa: Bernardette, Cecilia, Maria, Nadia, Susan na Teresia.

Sr. Maddalena, Sista Mkuu, alikaa siku kadhaa pamoja na Masista wetu hapa Ol Moran, hata baada ya sherehe.



*Kushoto:* Masista Wapya, baada ya ibada ya Nadhiri, pamoja na Baba Askofu Joseph na Sista Mkuu Maddalena.

*Baraka ya Familia na huduma nyingine*

## Karibuni Mashemasi

Mashemasi wawili wengine wametumwa kutoka Jimbo la Venisi katika Parokia yetu. Shemasi Daniele Cagnati na Shemasi Augusto Prinsen walifika kwetu tarehe 13 Februari, watakaa Parokiani hadi mwisho wa mwezi wa nne, ili wapate nafasi nzuri ya kujua kazi ya Kikanisa katika eneo letu na katika Jimbo la Nyahururu. Walifanywa kuwa Mashemasi na Askofu Mkuu wa Venisi, Patriarka Fransisko, mwezi wa kumi wa mwaka uliopita. Mungu akipenda, watakuwa Mapadri mwezi wa sita wa mwaka huu. Na katika Parokia yetu, wataendelea hata na kazi ya kubariki familia zetu kwenye maboma, pamoja na Parish Survey, iliyo kazi iliyoanzishwa mwaka uliopita na kikundi cha Mashemasi wengine. Walianza baraka za familia Alhamisi 27 Februari kule Githima. Baadaye watatembelea Kahuho na Ol Moran.







*MP Sara anaendeleza Shule za Serikali*

## Madarasa mapya Gathanji

Siku nzuri ya kusherehekea maendeleo ya elimu kwenye eneo letu ilikuwa Jumamosi 15 Februari. Katika Shule ya Msingi ya Gathanji yamefunguliwa rasmi madarasa sita yaliyojengwa na hazina ya NG-CDF. Shule ya Gathanji ilichaguliwa kwa ajili ya mradi huu kwa sababu ya matokeo mazuri ya KCPE ya miaka kadhaa iliyopita. Mradi huu ulisimamiwa na Mheshimiwa Sara Lekorere, MP Laikipia North, kufuatana na sera ya uongozi wake kwa ajili ya maendeleo ya elimu kwenye Laikipia North (#LaikipiaNorthElimuKwanza).

Sherehe ilihudhuriwa na raia wengi, pamoja na wanafunzi wa shule wa Gathanji na shule nyingine jirani. Mgeni wa Heshima, aliyefungua mradi, alikuwa Hon. Justine B. Muturi, Speaker of National Assembly. Wageni wengine waliokuwako ni Hon. Francis Ole Kaparo, Speaker Emeritus; Hon. John Mwaniki, Deputy Governor Laikipia; Hon. John Kinyua, Senator Laikipia; Hon. Patrick Mariru, MP Laikipia West; Hon. Mugambi Rindikiri, MP Buuri; pia MCAs wa maeneo yetu, Hon. Jacob Edong, Sosian, na Hon. George Karuiru, Ol Moran; na MCAs wa maeneo mengine.



*Juu:* MP Sara Lekorere, pamoja Mheshimiwa J. Muturi, wakifungua rasmi madarasa mapya ya Shule ya Gathanji.

*Kueneza Injili*

## Ziara ya Viongozi

Waakilishi wa Viongozi waliochaguliwa na PPC, pamoja na Mapadri, walikuwa na safari mbili za kutembelea vijiji vya maeneo ya Kaskazini ya Parokia. Nia ya ziara yao ilikuwa kujua hali ya Makanisa na Wakristu wa kule, pia mahitaji ya kikanisa ya yale maeneo yanayoendelea kupata wenyeji wapya. Viongozi walikwenda Jumanne 4 Februari katika vijiji vya Dam Mbili, Ndunyuriwo, Nakwam, Kanjul, na Lera. Tena, Jumanne 11 Februari walitembelea vijiji vya Posta, Silango, Maram, Kanambyo, Naibor, Postani.

Baada ya ziara yao, waakilishi watakutana na PPC nzima kujadiliana kuhusu mambo waliyoyaona na kusikia. Parokia lazima iamue jinsi itakavyofanya kazi ya kueneza Injili na kuendeleza maisha ya Kanisa hata pale.

*Kushoto:* Viongozi wa Parokia pamoja na wenyeji na walimu wa shule ya kijiji cha Kanjul.

*SSP: Parish Education Day, Jumamosi 21 Machi 2020*

## Hekima yatimiza miaka kumi

MIAKA KUMI YA HEKIMA - Mwaka 2010, tarehe 25 Machi, tulifanya sherehe ya kufungua nyumba ya wanafunzi "Hekima House". Nyumba ilifunguliwa rasmi na Baba Askofu Luigi Paiaro baada ya kuongoza ibada ya Misa pamoja na wanafunzi wa Hekima, wazazi wao, na wanafunzi wa Shule ya Upili ya Ol Moran High. Hata hivyo, kikundi cha kwanza cha wanafunzi tisa kilikuwa kimeingia mhula wa tatu wa mwaka 2009, baada ya kufanya kazi ya kutengenza upya mijengo ya Hekima. Hivyo ilianza maisha ya nyumba ya wanafunzi, iliyoendelea kupokea wanafunzi wa Ol Moran High School kwa hii miaka yote. Umefika wakati wa kusherehekea miaka kumi ya Hekima!

PARISH EDUCATION DAY - Kama mwaka uliopita, hata mwaka huu kutakuwa na Sherehe ya Elimu ya Kiparokia. Hiyo ni nafasi nzuri ya kusherehekea kazi ya elimu inayoendelezwa na Parokia kwa njia ya School Support Program, na kumshukuru Mungu pamoja. Itakuwa Jumamosi tarehe 21 Machi. Mwaka huu itafanywa Parokiani, ili tuweze kusherehekea kwa njia ya pekee miaka kumi ya Hekima House. Wamealikwa hata wazazi wa wanafunzi wa Hekima, pia wanafunzi wa Tumaini Academy, na waakilishi wa wanafunzi na walimu wa Ol Moran High School, Mithuri Secondary School, na wa shule jirani. Misa itaanza saa nne na nusu, na itaongozwa na Padri Samuel Amugori, aliyekuwa mkuu wa Ofisi ya Elimu ya Jimbo tulipofungua Hekima.

SAFARI YA HEKIMA - Kwa kukumbuka miaka kumi, wanafunzi wa Hekima wameshaanza kupanga safari yao ya mwaka pia: wakati huu wanatarajia kufika pwani, kule Mombasa. Wamepanga kazi mablimbali ya kusimamia gharama yake.





*Kulia juu:* Sherehe ya mwaka 2010, Askofu Luigi alipofungua rasmi Hekima House.
*Kulia chini:* Wanafunzi wa 2010, pamoja na Patron George na Matron Sara.

## Maombi ya Makanisa

Wakristu na Wachungaji wa Madhehebu mbalimbali ya Kikristu ya eneo letu walikutana kwa siku ya maombi pamoja Jumapili 16 Februari kijijini Ol Moran. Maombi yaliaanza saa tisa, yakiongozwa na wachungaji na waimbaji wa Makanisa. Ikawa nafasi nzuri ya kuiombea amani na umoja katika makanisa na pia katika jamii na eneo letu. Hata Mapadri wetu walishiriki, pamoja na Masista.

Tena, siku hiyo haikuwa ya maneno tu, bali kama ishara ya ushirikiano katika kazi ya huruma, Wakristu walichangia kwa nia moja mradi wa watoto wa Nyumba ya Magnificat, wanaopokelewa na Masista wetu.



*Kulia:* Wachungaji pamoja na washirika wa Makanisa kijijini Ol Moran.